MINISTRY MHUBIRI WA KIMATAIFA

# MHUBIRI

# WA

# MATAIFA

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha MHUBIRI WA MATAIFA. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

MHUBIRI WA MATAIFA

1.Mhubiri wa Mataifa?................................................

2. Kusudi la Huduma.................................................

3. Ubatizo..........................................................

4. Maombi...........................................................

5. Wokovu...........................................................

6. Mhubiri wa mataifa...............................................

7. Karama ..........................................................

8. Mke ..............................................................

9.Kuokoka...........................................................

10. Mwisho..........................................................

# 1. MHUBIRI WA MATAIFA ?

**Mhubiri wa mataifa** kwa kirefu ni Mhubiri wa injili kwa watu wa mataifa; ni huduma ya kanisa ya kuwahubiri **watu wa mataifa wenye dhambi** habari njema za Yesu mfufuka aliyesulubiwa na kumwaga damu yake kwa ajili ya wenye dhambi watubuo kwa jina lake wapate ondoleo la dhambi, wabatizwe kama Yeye na kujazwa Roho mtakatifu yaani wapate kuokoka.

Huduma hii ipo kwa ajili ya kulizidisha kanisa yaani watu waliokoka wanapokusanyika pamoja. Kuhubiri injili ni mojawapo ya kazi ya mungu aliyoifanya Yesu alpotumwa na Mungu au Baba yake duniani na ilitabiriwa na manabii na mpaka leo anafanya Yesu kupitia watumishi wake aliowatuma kama mitume,manabii na wahubiri; kanisa kwa agizo la Yesu kupitia mitume.

**Luka 4.18**

"Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta ku**wahubiri** maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa, "

**Marko 16.15** "Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, **mkaihubiri** Injili kwa kila kiumbe. "

Mhubiri wa mataifa umepewa neema na Yesu iwezayo kuokoa watu wa kila taifa ktk dunia wenye dhambi na wakaokoka na kumfuata Yesu na kuachana na maisha ya dhambi kabisa. Unaweza kwenda taifa hadi taifa kutamfuta mwanadamu aliyepotea ktk dhambi amrudie mungu apate kupatinishwa na Yesu si wewe peke yako bali na pamoja na Yesu.

## 2.KUSUDI LA HUDUMA

Kusudi la huduma ya Mhubiri wa mataifa ni kuwahuiri injili watu wa mataifa wenye dhambi wapate **kuokok**a na maisha ya dhambi. mfano ulevi, rushwa , zinaa ,anasa na kutokuamini. Na kupata wokovu.

**Rumi 10.13 - 14**

“kwa kuwa, Kila atakayeliitia Jina la Bwana **ataokoka.** Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo **mhubiri**? “

Yesu akikupa huduma utasimama mbele ya mataifa na kulishuhudia jina lake au kuhubiri injili wapo watakao ipokea na wapo watakaoipokea wewe utashikamana na wale watakao ipokea injili ndio Mungu aliotaka kumpa Yesu kupitia mhubiri wake.

Huna nafasi ya kusema na kanisa kwa sababu ya kusudi la huduma ya mhubiri wa mataifa ni kuokoka kanisa ni wenye haki mbele zaYesu ni waliookoka.

**Mathayo 9.13**

“Lakini nendeni, mkajifunze maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka; kwa maana sikuja kuwaita wenye **haki,** bali wenye **dhambi.** “

Yesu anaweza kukuita kwa huduma ya mhubiri wa mataifa siku chache au siku hiyo baada kuokoka akakupasha habari kwa roho mtakatifu wewe ni mhubiri wa mataifa au baada ya kuokoka ukiwa unamtumkia mungu na unataka kufahamu huduma iliyo ndani yako pengine karama za mungu unazifahamu funga na kuomba ili mungu akupashe habari ya huduma iliyo ndani yako omba hasa pindi ushirika wako na mungu unapokuwa mzuri mfano ulipojazwa roho mtatifu kwa ubatizo wa maji au kuwekewa mikono; ktk kumtumikia mungu sehemu ya ushirika na mungu ipo vizur kama maombi, maono,sauti ya yesu na roho mtakatifu,ndoto,maandiko,mawazo au ishara.

# 3. UBATIZO

Mtu uliyeokoka ukiwa umepewa na Yesu **huduma ya mhubiri** wa mataifa ni vizuri ukimfuata Yesu na mhubiri wa mataifa Paulo aliye kuwa na huduma zingine za kanisa kama ya utume na ualimu. (Biblia)

Kwa habari ya ubatizo ya maji mhubiri Paulo wa Mataifa hakutumwa kubatiza kwa maji alipobatiza tatizo lilitokea ndani ya kanisa . Yeye alitumiwa na Yesu kubatiza wale watubuo kwa kuwekea mikono wapokee roho mtakatifu na karama.

**1 kor 1: 11-17**

"... nimearifiwa habari zenu na wale walio wa nyumbani mwa Kloe, ya kwamba iko fitina kwenu. ..., Mimi ni wa Paulo, na, Mimi ni wa Apolo, na, Mimi ni wa Kefa, na, Mimi ni wa Kristo. Je! Kristo amegawanyika? Je! Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu? Au je! Mlibatizwa kwa jina la Paulo? Nashukuru, kwa sababu sikumbatiza mtu kwenu, ila Krispo na Gayo; ... Tena naliwabatiza watu wa nyumbani mwa Stefana; .... Maana Kristo hakunituma ili nibatize."

Ukimfuata Yesu na Mhubiri Paulo wa Mataifa ukiwa nawe upewa na Yesu huduma ya mhubiri ya Mataifa utamwomba Yesu akutumie kuwabatiza kwa roho mtakatifu wale wamkiri Yesu ni Bwana kuokoka kwa kuwawekea mikono wapokee **Roho mtakatifu** na **karama.**

**Matendo 19: 1— 7**

"Ikawa, Apolo alipokuwa Korintho, Paulo, akiisha kupita kati ya nchi za juu, akafika Efeso; akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko; akawauliza, Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini? Wakamjibu, La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia. Akawauliza, Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani? Wakasema, Kwa ubatizo wa Yohana. ...." Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, **Roho Mtakatifu** akaja juu yao; wakaanza **kunena kwa lugha,** na **kutabiri.** .."

# 4. MAOMBI

Maombi unayotakiwa kuwa nayo mtumishi wa Yesu uliyepewa huduma ya mhubiri wa Mataifa siku zote za wokovu wako na kadri Roho mtakatifu atakavyokuongoza ktk kweli ili upate kupelekwa na Yesu au na huyo Roho mtakatifu ni:

- Kuowaombea watu wa mataifa waliokusudiwa kuokoka kupitia wewe waokoke kila siku ktk nchi mbalimbali duniani maana hayo ndiyo mapenzi ya mungu yaliyotimia mbinguni yanayotakiwa kutumia duniani sawa sala aliyowafundisha mitume walipomwomba Yesu awafundishe kusali. **Math 6 :10**
- Kuomba uokolewe na wataabishao na wasioamini ktk nchi yako na nchi mbalimbali Yesu anapokupeleka kuhubiri injili kwa watu wa mataifa. Wenye dhambi waliokusudiwa na mungu kuokoka.
- Kuwaombea wale waokokao wadumu ktk imani ya Yesu na kuzaa matunda kanisa lolote la waliokoka watakapoenda kumwabudu Yesu na kuishi na wenzao ktk wokovu kwa amani.
- Kuomba Yesu akutumie kuokoa watumishi wa mungu kama wewe wenye huduma kubwa za kanisa kama mitume, manabii, wainjilisti, mwalimu,wachungaji na wengineo kama watenda miujiza, waponyaji,viongozi,waimbaji,wahubiri,waombaji,Matajiri wachangia injili ya Mungu, wabarikiwa n.k
- Kuombea maisha yako yawe na ushuhuda kwa mungu na kwa watu , matakatifu na yenye usafi wa roho na mwili. Uletwao na hekima kama matokeo ya kuyapokea mema moyoni yatokayo kwa Yesu. Wokovu wako unatakiwa kutenda amri za mungu, kuhubiri, kumcha mungu ,kuishi maisha ya toba na kutenda mema kama Yohana mbatizaji alivyowafundisha watubuo **luk 3 : 10—14**
- Kuomba Yesu ainue huduma yako mpaka kufikia kuwa na uwezo Yesu kukutumia kwa mikutano ya injili kwa watu wa mataifa.

## 4.WOKOVU

Wokovu wa mhubiri wa mataifa lazima ushike na kutenda mambo yafuatayo yaliyoayomo ktk biblia takatifu:=>

- Amri za Mungu na Yesu

Kushika na kuzitenda amri za mungu na Yesu ni lazima ukivunja usipotubu laana iko inakuatilia au fimbo ya Yesu kwa u mtoto mbele za Baba yake Yesu.

- Kumhubiria mwenye dhambi aokoke

Kuhubiri kwako ni kazi mbali na kuwa huduma kumbuka Mungu aliwaambia waisraeli wafanye kazi siku sita na ya saba ni ya Bwana ni sabato wasifanye kazi.Kuhubiri kama kazi unatakiwa kutimiliza huduma yako ktk siku sita na ya saba ni ya Bwana Yesu.

- Mche Mungu

Kumcha mungu ni kuchukia uovu kama kiburi , majivuno na njia mbovu au mbaya .Huko kunatunza upako ulio juu yako.

- Maisha ya Toba

Ukimkosea mungu mfano kuvunja amri zake labda hujashika sabato kimbilia toba. Tubu kosa lako na usilirudie.

- Kutenda mema anzia kanisa

Uwe mwema kwa watu wa kanisani kwako akopaye kwako mfadhili msimpe kisogo uwe mkweli kama huna mwambie sina .

- Yale mema unayowahubiri nawe uyatendee kazi.

Hayo mambo ya muhimu ktk wokovu wa mhubiri wa mataifa ambayo ukiyashika na kuyatenda mungu anakupenda. Ukimwomba lolote lililo sawa na mapenzi yake anakupa kufumba na kufumbua kwa kuwa unayashika ya kwake na kuyatenda.

## 5. MHUBIRI WA MATAIFA

Ktk biblia mtumishi wa Yesu mwenye huduma ya **Mhubiri wa mataifa :=>**

Ni **mhubiri,**mwalimu na mtume **Paulo wa mataifa** mojawapo ya huduma ya kanisa iliyo ndani yake ni ya **mhubiri wa mataifa.**

**1 timotheo 2:7**

“Nami kwa ajili ya huo naliwekwa niwe **mhubiri** na mtume,... mwalimu **wa Mataifa** katika imani na kweli. “

Ukipewa na Yesu huduma moja na Yesu ya mhubiri wa mataifa ufahamu utakwenda taifa hadi taifa kuhubiri injili kwa wenye dhambi watu wa mataifa waokoke maana yake watoke kutoka ktk maisha ya dhambi Yesu atakutumia kuwaokoa nakukupeleka au roho mtakupeleka ukikaa ktk maombi utasikia sauti ya roho mtakatifu ya kukupeleka kuhubiri Yesu . Kama ni Yesu wakati mwingine anaweza kukutokea na kukupeleka.

Unayetakiwa kumfuate ni Yesu na Paulo kama una huduma moja ya mhubiri wa mataifa.Huduma yoyote ya mhubiri ukipewa na Yesu ina heri na ole kwa kuokoka. Paulo anasema ole wangu nisipoihubiri injili

**1kor 9:16**

Maana, ijapokuwa naihubiri Injili, sina la kujisifia; maana nimewekewa sharti; tena ole wangu nisipoihubiri Injili!

Ukihubiri yapo mema utapata **ridhiki** usipohubiri utapatikana na **mabaya.**

# 7. KARAMA

Karama apewazo mhubiri wa mataifa a ni kama zile alizopewa mhubiri Paulo wa Mataifa au Mhubiri wa injili Filipo ktk biblia unaweza kuwasoma na kuwatafakari nazo ni:

1)Hekima 2)Miujiza 3)Uponyaji 4)Kunena kwa lugha

Lakina Yesu huwapa **amri ya kutoa pepo** au **mamlaka ya kutoa pepo** na **nguvu za giza** ya juu kuliko wengine.

Hayo yote Yesu humkirimia mtumishi wake ili aliyempa huduma ya mhubiri wa kimataifa apate kumtumia kuwahubiri injili watu wa kimataifa kwa hekima , kuwatendea miujiza na kuwaondolea laana ya magonjwa waokokao kwa kuwaponya magonjwa yao. Na kuwatoa pepo na nguvu za giza zilizokuwa zinawamiliki kabla ya kuokoka..

Kumwomba Roho mtakatifu akundishe namna ya kuzitumia kila unapokwenda kuhubiri ni muhimu maana kupitia hizo Mungu hujidhihirisha watu wa mataifa wenye dhambi na jina la Yesu hutukuzwa mbinguni.

**Matendo 19:11— 12**

"Mungu akafanya kwa mikono ya Paulo **miujiza** ya kupita kawaida; hata **wagonjwa** wakaletewa leso na nguo zilizotoka mwilini mwake, magonjwa yao **yakawaondokea**, **pepo wachafu** wakawatoka. "

**1 timotheo 2:7**

"Nami kwa ajili ya huo naliwekwa niwe **mhubiri** na mtume,... mwalimu **wa Mataifa** katika imani na kweli. "

Ktk maandiko hayo juu Mhubiri Paulo wa mataifa ktk utumishi wake zinaonekan a karama mbili na amri ya kutoa pepo nazo ni miujiza na uponyaji (wagonjwa magonjwa **yakawaondokea**—ni karama ya uponyaji.)

## 8. MKE

Kwa habari ya mke ukimfuata Yesu na mhubiri Paulo wa mataifa utakaa bila kuoa bali ukiufuata ushauri wa Mwalimu wa kanisa Paulo swali la kujiuliza ni hili Je una neema ya kukaa bila kutamani mwanamke kama Yesu au Paulo? Je Mwili wako hakufundishi? Je unasumbuliwa na tamaa ya mwili?Maumbile ya mwili wako hayakufundishi?

Kwa sababu ya zinaa kama maumbile ya mwili wako yanakufundisha au unasumbuliwa na tamaa ya mwili kuoa ni lazima siyo hiari.

Kama una huduma ya Mhubiri wa mataifa huna neema ya kukaa bila kuoa kama Yesu au Paulo na mwili wako huwaka tamaa kuoa ni lazima kwako usimfuate Yesu kwa kutokuoa au Paulo bali fuata mafundisho ya Yesu kuhusu mke ukawe naye Mmoja sikuzote za maisha na kupokea baraka ya mungu ya watoto kama mungu alivyowabari Adamu na mkewe hapo mwanzo wa uumbaji wakamzaa Habili na Kaini.

**Mwanzo 1:27—28**

"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba.

Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi. "

**Mwanzo 4:1 –2**

Adamu akamjua Hawa mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Kaini, akasema, Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana.

Akaongeza akamzaa ndugu yake, Habili. Habili alikuwa mchunga kondoo, na Kaini alikuwa mkulima ardhi.

# 9. NABII

Nabii ni nani? Ni mtu anayeoneshwa/sikizishwa jambo linaloweza kutukia/kutendwa baadaye na la kweli na Baba yake Yesu au Mungu. Na kweli hutukia unabii hutoka kwa mungu. Tafsiri ya neno nabii ni mwonaji.

Yesu ni nabii mkuu aliyetabiria mitume mabaya yatakayowapata kwa ya kuhubiri injili yake ; Unyakuo wa kanisa na mwisho wa dunia au Dahari. Aliyetabiria waokokao kutambulika kwa ishara na watumishi wake kwa kazi, waokokao kujibiwa maombi yao na kujenga kanisa, ujio wa msaidizi Roho mtakatifu na ikawa kwa waliokoka.

**Yoh 16.2 "Watawatenga na masinagogi; naam, saa yaja atakapodhania kila mtu awauaye ya kuwa anamtolea Mungu ibada."**

**Math 23.34— 35 "Kwa sababu hiyo, angalieni, mimi natuma kwenu manabii na wenye hekima na waandishi; na wengine wao ninyi mtawaua na kuwasulibisha, na wengine wao mtawapiga katika masinagogi yenu, na kuwafukuza mji kwa mji; hivyo ije juu yenu damu yote ya haki iliyomwagika juu ya nchi, tangu damu ya Habili, yule mwenye haki, hata damu ya Zakaria bin Barakia, mliyemwua kati ya patakatifu na madhabahu."**

**Marko 13.9 Nanyi jihadharini nafsi zenu; maana watawapeleka ninyi mabarazani; na katika masinagogi mtapigwa; nanyi mtachukuliwa mbele ya maliwali na wafalme kwa ajili yangu, kuwa ushuhuda kwao.**

**Matendo ya Mitume 9:1 – 2 Lakini Sauli, akizidi kutisha na kuwaza kuwaua wanafunzi wa Bwana, akamwendea Kuhani Mkuu, akataka ampe barua za kuenda Dameski zilizoandikwa kwa masinagogi, ili akiona watu wa Njia hii, waume kwa wake, awafunge na kuwaleta Yerusalemu.** Mistari ya maandiko hayo inathibitisha Yesu ni nabii alitabiri na yakawa mf: mistari ya matendo utimiaji wa nabii zake.

## 10. AMRI YA KUTOA PEPO NA NGUVU ZA GIZA

Yesu ana amri ya kutoa pepo wa kila aina leo twashuhudia kwa jina lake nguvu za giza hutolewa kama uchawi, uganga wa kienyeji, utendaji wa falme au mamlaka za giza husimamishwa au kuharibiwa.

**"Math 12.28 Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia."**

Yesu alitoa pepo kwa nguvu za Roho mtakatifu yaani nguvu za mungu amri yake ya kutoa pepo iliambatana na nguvu za mungu . Siyo maneno matupu yenye amri yasiyo na nguvu za mungu.

**"Math 17.18 Yesu akamkemea pepo, naye akamtoka; yule kijana akapona tangu saa ile."**

Andiko hili linashuhudia Yesu ana amri ya kutoa pepo wanaotesa wanadamu. Kwa mtu uliyeokoka wa kimataifa Yesu yu ndani yako fahamu una amri ya kutoa pepo si wewe bali Yesu aliye ndani yako Marko 16;14-18

**"Marko 1:25—26 Nakutambua u nani, Mtakatifu wa Mungu. Yesu akamkemea, akisema, Fumba kinywa, umtoke.Yule pepo mchafu akamtia kifafa, akalia kwa sauti kuu, akamtoka."**

**"Marko 1.34 Akaponya wengi waliokuwa na maradhi mbalimbali, akatoa pepo wengi, wala hakuwaacha pepo kunena, kwa sababu walimjua."**

**Marko 3.11 Na pepo wachafu, kila walipomwona, walianguka mbele yake, wakalia wakisema, Wewe ndiwe Mwana wa Mungu.**

Kwa mistari michache ya maandiko matakatifu inashudia Yesu alikuwa amri ya kutoa Pepo. Akiwa ndani yako ujue una amri ya kutoa pepo. Kutoa pepo ni sehemu ya maisha ya Yesu alipokuwa ktk dunia. Ukitoa pepo kwa jina lake kama kifafa ufahamu yu ndani yako na yu upande hiyo kazi ya mungu unayofanya.

## 9.HANA DHAMBI

Yesu hana dhambi maisha yake yalikuwa makamilifu mbele za mungu kwa kuitii sauti yake , haikuonekana hila ktk midomo yake wala moyoni.. Pia hakuna mwanadamu aliyeweza kushuhudia kuwa ana dhambi. Wokovu wa Yesu hakuwa dhambi alikuwa mkamilifu ktk kushika yaliyoandikwa ktk torati na yaliyoamriwa na mungu kwa kutumia manabii wake,Kwa kuwa alikuwa hana dhambi chochote chenye asili ya dhambi kama umaskini. Ugonjwa, mapepo. Nguvu za giza uchawi na kazi yoyote ya yule mwovu alikuwa na mamlaka juu ya hizo kama kuziharibu,kuzitoa au kuzibomoa kwa nguvu roho mtakaifu na kwa jina la Baba yake.

**Yoh 8.34—36 "Yesu akawajibu, Amin, amin, nawaambia, Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi.Wala mtumwa hakai nyumbani sikuzote; mwana hukaa sikuzote. Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli."**

Kwa maneno ya kinywa chake ktk maandiko hapo juu Yesu hakuwa mtumwa wa dhambi. Alikuwa huru mbali na dhambi,alikuwa haitumikii dhambi.

**Yoh 8.46 "Ni nani miongoni mwenu anishuhudiaye ya kuwa nina dhambi? Nami nikisema kweli, mbona ninyi hamnisadiki?"**

Kwa maneno ya kinywa chake ktk maandiko hapo juu Yesu hakuwa na dhambi kabisa.

**1 Petro 2:22 – 23 "Yeye hakutenda dhambi, wala hila haikuonekana kinywani mwake.**

**Yeye alipotukanwa, hakurudisha matukano; alipoteswa, hakuogofya; bali alijikabidhi kwake yeye ahukumuye kwa haki."**

Kwa maneno ya kinywa chake ktk maandiko hapo juu Yesu hakutenda dhambi ktk maisha yake hata kama alionewa hakutoa maneno ya hila hila kinywani mwake. Kama umeokoka mtafute Yesu akuweke huru siku zote ktk wokovu wako ndipo utakuwa mwana kweli.

## 10. YESU ANASEMA

Yesu anasema na kondoo wake nao humsikia. Kondoo wake ni watu waliokoka kama wewe mtu wa kimataifa uliyeokoka unaposikia sauti yake itii kama ya mfalme,Bwana au mchungaji wako ujue anakuongoza kukupeleka ktk malisho na mahali yalipo maji yaliyo hai . Kuitii sauti yake ni ya lazima upate kuzipokea baraka zake alizokubariki rohoni bali usipotii ufahamu laana inakufuatilia usiseme wokovu mgumu.

**"Yoh 10.27 Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata.**

**"Yoh 10.28 Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu."**

**"Yoh 10.29 Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote; wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu."**

Wewe ni kondoo wa Yesu mtu wa kimataifa uliyeokoka na Yesu ni Mchungaji wako mwema na Mkuu. Umejaliwa kusikia sauti ya Yesu .Yesu amekuja kuishi nawe ili akujaze uzima tele na kukulinda dhidi ya yule mwovu u mikononi mwa Baba yake ndiye mungu ili baada ya maisha ufike kwake ktk makao aliyoiandaa na kuishi nawe.Umekusudiwa uzima/mema na Mungu na Yesu.Mwombe Yesu siku zote akuongeze kwa sauti yake. Kwa kutii mafundisho yaliyo ktk injili ya mathayo,marko,luka na yohane ya ktk biblia unaitii sauti ya Yesu.

Kama umeokoka na umejaliwa kusikia ya mungu ya rohoni Ukiwa huna dhambi sauti ya Yesu ikisema ktk moyo wako kwa utukufu wa kumuona au kutokumuona hushuhudiwa na roho mtakatifu kuwa anayesema nawe ni Yesu ina Msusumo/msukumo(upendo) yenye pumzi ya uzima au maisha ya milele ya upole na nyenyekevu lazima kuitii usitoe udhuru kwa kutazama yanayokuzunguka au changamoto. Yesu anasema ili awe mchungaji wako yapasa umtii.

# 11. AMEJAA AMANI,FURAHA,UPENDO,HAKI

Ukweli ewe mtu wa kimataifa uliyeokoka maisha yako yamejaa nuru kwa sababu huyo Yesu uliyempokea ndiye nuru. Maisha yako hayana giza tena uovu umeondolewa.

**Yohana 8.12**

**“ Basi Yesu akawaambia tena akasema, Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.”**

Maisha yako yana nuru ya uzima unapaswa kumfuata yesu kwa kutii neno lake. Baadhi ya maneno aliyosema Yesu yamo ktk vitabu vinne vya injili ktk biblia navyo mathayo,luka,marko na Yohana. Penda kusoma na kutafakari mema yaliyomo ktk maandiko ya vitabu hivyo vya injili na uyatendee kazi utapata Imani ya kweli ya Yesu yenye msingi imara.

**1Yoh: 1.5 — 7**

“Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake, na kuihubiri kwenu, ya kwamba Mungu ni nuru, wala giza lo lote hamna ndani yake.

Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli;

bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote”

Tunza hiyo nuru kwa kushirikiana Roho mtakatifu ktk kutenda yaliyo haki pachoni pa mungu wa mbinguni baba yake Yesu. Usiifiche iweke wazi yaani tangaza wokovu wako kwa matendo na maneno. Luk 8:16

# 12. AMEJAA UZIMA TELE

Msaidizi wako ewe uliyeokoka mtu wa kimataifa ktk maisha yako ya wokovu ni Roho mtakatifu. Huyu ulimpokea pindi ulipookoka ya siku ile ulipookoka au kubatizwa kwa roho mtakatifu.

Roho mtakatifu aliye ndani yako anatoa usaidizi ktk mambo yafuatayo:

- Kukufundisha na kukumbusha yote yatokayo kwa yesu.

Kukufundisha biblia ukimwombwa andiko lilio ktk injili akufundishe usiloliewa atakufundisha.

- Kumshuhudia Yesu ndani yako

Roho mtakatifu humshuhudia yesu ktk maisha yako kwa kukutendea makuu ya Yesu na kukutumia kuwatendea wengine makuu. Mfano kutoa pepo au kuponya.

- Kuhakikishi ulimwengu juu dhambi,haki na hukumu

Ukienda kuhubiri wenye dhambi roho mtakatifu aliye ndani yako huta sana huo usaidizi akishirikiana nawe. Kuwa Yesu ndiye mwenye haki , wanadamu wote wametenda dhambi, upo moto wa jehanamu kwa watakaokataa kuokoka kwa jina Yesu.

- Kukuongoza ktk kweli

Roho mtakatifu anakusaidia kukuongoza utii maneno ya mungu ktk yale unayotenda ya kila siku.

- Kukushauri ushauri utokao kwa Yesu ktk yale unayopitia
- Kukupasha habari juu ya mambo yajayo yatokayo kwa Yesu.

Mambo mema ambayo Yesu amekuandalia roho mtakatifu hukupasha habari ktk maono,sauti ya ndani ya roho yako,kupitia watumishi wa mungu.

# 13. MFALME

Kuokoka ni kuzaliwa mara pili mbinguni kwa maji na kwa roho; ni kutubu, kubatizwa kwa maji mengi na kujazwa roho mtakatifu.Yoh 3 : 5 — 7

**“Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.**

**Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho.**

**Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili.”**

Roho imezaliwa upya kwa njia ya Roho mtakatifu kama mtoto alivyozaliwa duniani na mwili ndivyo ulivyozaliwa ktk roho mbinguni mbele za mungu.

**Luk 10.20**

**“Lakini, msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni.”**

Upo mbinguni tangu uokoke mtu wa kimataifa jina lako lime-andikwa kule baada ya kupewa wenyeji wa kule mbinguni una mamlaka dhidi ya pepo wachafu

**Marko 16:14-18**

“..**Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;..”**

Roho yako uliyeokoka mtu wa kimataifa ipo mbinguni bali mwili wako kwenye dunia, roho yako ipo kule ili ipokee ya mbinguni yanayotakiwa kuzidhirika ktk dunia sawa

**Mathayo 6:10“Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.”**

## 14. MFALME

Mtu wa kimataifa  uliyeokoka wewe ni umpewa uwezo wa kuwa mwana wa mungu umepewa haki kama ya Yesu mbele za mungu yakutwaa urithi wake alipewa na ulioshuhudiwa ktk maisha yake ya kwenye dunia kwa sehemu ya kutumiwa na mungu ktk kutenda makuu na kuishi bila kutenda dhambi.

**Yohana 1:12**

**“Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake;”**

**Wagalatia 4.6 - 7**

**“Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba.**

**Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu.”**

Mtu wa kimataifa  uliyeokoka  umefanyika mwana roho mtakatifu uliyepewa tafuta mafundisho yake na jifunze habari zake kimatendo kwa kuyatii mafundisho yake ili upate ufahamu juu ya msaidizi aliye ndani yako anavyowasiliana/shirikiana nawe ktk kutoa usaidizi upate kuwekwa huru dhidi ya dhambi na Yesu ili ufurahie wokovu wako ewe mtu wa kimataifa uliyeokoka.

**Waebr 12:6  “Maana yeye ambaye Bwana ampenda, humrudi, Naye humpiga kila mwana amkubaliye.”**

Kwa kuwa u mwana Mtu wa kimataifa  uliyeokoka  epuka/kataa kufanya makossa/dhambi kuna fimbo kutoka kwa Yesu asije akakupiga kwa kufanya dhambi wokovu wako ukawa huna furaha.Mtoto ana haki ya kupigwa fimbo akifanya kosa apate kujirekebisha

## 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**

Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :

**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 9332

**MWENGE— DAR-ES-SALAAM TANZANIA**



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha


Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034